

Maswali

1. Mwanzoni Paulo alipoenda Rumi, alikubaliwa kukaa wapi?
2. Nani alichunga Paulo usiku na mchana?
3. Paulo alifanya nini alipokuwa akikaa kwa nyumba ya kukodisha?
4. Mtumwa aliyekuwa ametoroka, akaamini na akabatizwa alikuwa nani?
5. Paulo aliandikia nani aliporudisha Onesimo?
6. Mbona Paulo alikuwa pekee yake alipopelekwa mbele ya Kaisari Nero?
7. Nani alikuwa karibu na Paulo akimsaidia?
8. Zaidi Paulo alitaka kuona nani?
9. Paulo alitaka Timotheo amletee nini?
10. Paulo aliuawa. Nini itafanyika kwa Paulo wakati Yesu atarudi?

Majibu

1. Paulo alikubaliwa kukaa kwa nyumba iliyokodishwa.
2. Askari wa Kirumi alichunga Paulo usiku na mchana.
3. Paulo alihubiri Injili kwa kila mtu aliyekuja kumwona.
4. Onesimo ni mtunwa aliyetoroka lakini aliamini na alibatizwa.
5. Paulo aliandikia Filemoni. Onesimo alikuwa mtumwa wa Filemoni.
6. Marafiki wa Paulo wote waliogopa na wakamtoroka.
7. Mungu na Bwana Yesu walikaa karibu na Paulo na walimsaidia
8. Paulo alitaka kumwona Timotheo zaidi kwa sababu alikuwa kama mwanawe.
9. Paulo alitaka Timotheo amletee joho yake na vitabu vya ngozi.
10. Yesu atafufua Paulo kutoka kwa wafu. Atasaidia Yesu kutawala ulimwengu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



102 Paulo ako Rumi

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume 28: 11 – 31; 2 Timothy 4:6 – 18; Filemoni

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo aliendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu wakati alikuwa gerezani na alipokuwa karibu na kifo. Mungu alikuwa karibu na Paulo na atafufuliwa kuishi kwa Ufalme wa Mungu wakati Yesu atarudi.

Somo

Paulo alisafiri salama kutoka Malita mpaka Italia. Paulo alichukuliwa na wafungwa wengine mpaka Rumi. Alikaa Rumi kama mfungwa kwa zaidi ya miaka miwili.

Mwanzoni Paulo alikubaliwa kukodisha nyumba yake. Aliishi kwa nyumba yake ya kukodisha lakini askari wa Kirumi alikaa naye akimchunga usiku na mchana. Marafiki wake walikubaliwa kuja kumuona. Paulo alikubaliwa kuwafundisha Injili. Watu wengi, Wayahudi, watu wa Mataifa na Wakristo walikubaliwa kuja kumuona. Aliwahubiria habari njema juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu utakaokuja duniani. Watu wengi waliamini na wakabatizwa. Watu wachache kutoka kwa nyumba ya Kaisari waliamini Injili na wakawa Wakristo.



Onesimo alikuwa mtumwa aliyetoroka. Alienda Rumi kwa nyumba ya Paulo. Onesimo alisikiliza Paulo. Aliamini Injili na akabatizwa. Onesimo alikuwa mtumwa wa Filemoni rafikiye Paulo. Onesimo alikuwa ametoroka Rumi. Ilikuwa jambo mbaya sana mtumwa kutoroka. Angeadhibiwa vibaya sana. Angeuawa.

Paulo aliamua kurudisha Onesimo kwa Filemoni. Paulo alirudisha Onesimo na barua. Paulo aliuliza Filemoni amusamehe kwa kutoroka. Alimuuliza amuchukue kama mtumwa wake tena. Kwa sababu sasa alikuwa nduguye Filemoni katika Kristo. Paulo alikuwa mzuri aje! Alikuwa mtumwa lakini alijali ndugu na dada zake. Alikuwa mzuri kwa Onesimo mtumwa aliyetoroka. Tunaweza kusoma barua yenye Paulo aliandikia Filemoni katika Agano Jipya.

Baadaye mambo hayakuendea Paulo vizuri. Aliwekwa gerezani. Wakati mwingine Paulo alitendewa vibaya. Wengi wa marafiki zake walienda wakamwaacha. Paulo alikuwa na upweke.



Kaisari Nero

Paulo alipelekwa kwa Kaisari kuhukumiwa. Marafiki wa Paulo waliogopa wakati alipopelekwa mbele ya Kaisari mara ya kwanza. Wote walimwaacha. Paulo hakukuwa na yeyote wakumsaidia. Paulo alihukumiwa na Kaisari Nero aliyekuwa mkatili sana. Yesu alikuwa karibu na Paulo. Mungu na Yesu walimsaidia Paulo na kumtuliza. Paulo aliachiliwa kwa muda.

Paulo alijua kwamba hana muda mwingi wa kuishi. Alitamani kuona marafiki zake kabla afe. Paulo sasa alikuwa mzee. Zaidi alitaka kumwona Timotheo. Paulo hakukuwa na watoto wake. Timotheo alikuwa kama mwanawe. Paulo aliandikia Timotheo barua. Alimpa moyo wakuendelea kuhubiri Injili. Paulo alitaka Timotheo aje amwone.

Paulo aliuliza Timotheo amletee joho imzuie kwa baridi. Zaidi, alitaka Timotheo amletee vitabu hasa vya ngozi. Paulo alikuwa anaendelea mwisho wa maisha yake. Aliumia sana wakati huu. Lakini hakujijali. Aliendelea kuandikia marafiki zake Wakristo. Alikuwa amebatiza Wakristo wengi. Alikuwa ameimarisha vikundi vingi vya Wakristo waaminifu. Paulo alitaka kuwaandikia. Alitaka kuwapa moyo ili waendeleo kukaa waaminifu kwa Mungu. Paulo alipokuwa Rumi, aliandika barua nyingi. Tunaweza kusoma barua zake kwa Timotheo. Tunaweza kusoma barua zake zingine alizoandikia makanisa ya Wakristo. Hizi barua ziko kwa Agano Jipya.



Paulo alirudishwa kwa Kaisari tena. Alihukumiwa kifo. Labda alitolewa nje ya Rumi ndiyo akakatwa kichwa. Lakini hii sio mwisho wa hadithi ya Paulo. Hakuogopa kifo. Paulo alikuwa amepigania Yesu vita vizuri. Imani alikuwa ameiweka. Paulo alijua taji ya haki ilikuwa imemuongojea. Hivi karibuni Yesu atarudi duniani. Yesu atamfufua Paulo kutoka kwa wafu na ataishi milele kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani. Paulo atasaidia Yesu kutawala ulimwengu.